

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA JIJINI MBEYA (“MBEYA WSSA”) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-009

Mnamo tarehe 6 Julai 2018, Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya jijini Mbeya (Mbeya WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi na majitaka kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 hadi 8 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za Sasa na Zilizopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Matumizi ya Sasa	Matumizi yaliyopen dekezwa	Bei za Sasa	Bei Zilizopendekezwa					
			2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	0-5	0-10	670	72%	1,150	13%	1,300	12%	1,450
	5--15	10--20	720	75%	1,260	7%	1,350	11%	1,500
	>15	>20	820	77%	1,450	0%	1,450	10%	1,600
Taasisi	0--30	0--30	820	107%	1,700	6%	1,800	14%	2,050
	>30	>30	920	104%	1,880	9%	2,050	10%	2,250
Biashara	0-20	0-30	920	85%	1,700	6%	1,800	14%	2,050
	>20	>30	920	104%	1,880	9%	2,050	7%	2,200
Viwanda	0-50	0-50	1,070	83%	1,960	5%	2,050	7%	2,200
	>50	>50	1,250	72%	2,150	2%	2,200	9%	2,400
Kioski	Block	Block	500	100%	1,000	0%	1,000	0%	1,000
Bulk	Block	Block	500						
Boza	Block	Block	2,800	7%	3,000	0%	3,000	0%	3,000

Jedwali 2: Tozo za Sasa na Zilizopendekezwa za Kurejeshwa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa Marejesho).

Kundi la Wateja	Tozo za Sasa	Tozo Zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	12,000	67%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Taasisi	18,000	67%	30,000	0%	30,000	0%	30,000
Biashara	18,000	67%	30,000	0%	30,000	0%	30,000
Viwanda	23,000	74%	40,000	0%	40,000	0%	40,000

Jedwali 3: Ada za Sasa na Zilizopendekezwa za Fomu ya Maombi ya Kuunganishiwa Huduma ya Maji (Shilingi kwa Fomu).

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	10,000	100%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Biashara	10,000	150%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Taasisi	10,000	150%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Viwanda	10,000	150%	25,000	0%	25,000	0%	25,000

Jedwali 4: Ada za Sasa na Zilizopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Majisafi (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa
Taasisi							
Biashara							
Viwanda							

Jedwali 5: Ada za sasa na zilizopendekezwa kwa wateja waliunganishiwa na huduma ya Maji safi na Majitaka (Shilingi kwa mita za ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	290	33%	385	0%	385	0%	385
Taasisi	350	43%	500	0%	500	0%	500
Biashara	400	44%	575	0%	575	0%	575
Viwanda	490	43%	700	0%	700	0%	700

Jedwali 6: Ada za sasa na zilizopendekezwa kwa wateja wasio unganishiwa na huduma ya Maji safi (Shilingi kwa mita za ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	10000	100%	20000	25%	25000	0%	25000
Taasisi	12000	233%	40000	13%	45000	0%	45000
Biashara	18000	122%	40000	13%	45000	0%	45000
Viwanda	18000	178%	50000	20%	60000	0%	60000

Jedwali 7: Ada za sasa na zilizopendekezwa kwa huduma za Majitaka za Boza (Shilingi kwa Boza)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	35000	29%	45000	11%	50000	10%	55000
Taasisi	35000	29%	45000	11%	50000	10%	55000
Biashara	35000	29%	45000	11%	50000	10%	55000
Viwanda	35000	29%	45000	11%	50000	10%	55000

Jedwali 8: Gharama ya Huduma ya Sasa na Iliyopendekezwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	2000	-100%	0	0%	0	0%	0
Taasisi	2500	-100%	0	0%	0	0%	0
Biashara	2500	-100%	0	0%	0	0%	0
Viwanda	10000	-100%	0	0%	0	0%	0
Kioski	0	N/A	0	0%	0	0%	0

Kutokana na wasilisho la Mbeya WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, gharama za watumishi, kusaidia miradi ya uwekezaji maeneo ya Mbalizi Mjini na viunga vyake, tathmini ya athari za mazingira, fidia na ujenzi wa mradi, kubadilisha takriban mita 13,000 na kuimarisha Ulinzi wa vyanzo vya maji 13 vilivyopo.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 16 Agosti, 2018**, katika Ukumbi wa **Mkapa** jijini Mbeya kuanzia saa 4:00 asubuhi ili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la Watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **30 Agosti, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI YA EWURA NYANDA ZA JUU KUSINI, GHOROFA YA NNE, JENGO LA NHC, ENEO LA UHINDINI, MBEYA**, au ofisi za Mbeya WSSA zilizo jijini Mbeya.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
2 Agosti 2018